# Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara (FAQs)

SAMIA INFRASTRUCTURE BOND

**1) Hatifungani ni nini?**
Hatifungani ni aina ya uwekezaji ambapo mwekezaji anawekeza katika taasisi (shirika au Serikali) kwa kuikopesha fedha kwa muda na riba maalum.

**2) Nini tofauti kati ya kuwekeza katika Hatifungani na kuweka fedha katika akaunti ya muda maalum?**

- Unapowekeza katika Hatifungani, unaikopesha fedha zako benki/taasisi inayotoa Hatifungani. Hivyo, unakuwa hauweki fedha katika akaunti ya mteja.
- Hatifungani ya CRDB inaweza kuuzwa katika Soko la Hisa la Dar Es Salaam (DSE) kabla hata ya ukomavu wake na mshika Hatifungani/mwekezaji atalipwa kiasi cha awali na Kuponi yoyote iliyolipwa hadi muda huo tofauti na akaunti ya muda maalum.
- Hatifungani ya CRDB inalipa kuponi mara mbili hadi nne kwa mwaka na sio hadi kufikia kipindi cha kuiva kwa Hatifungani kama ilivyo kwa akaunti ya muda maalum

**3) Hatifungani ya Miundombinu ya Samia ni nini?**
Hatifungani ya Miundombinu ya Samia ni aina ya uwekezaji wa Hatifungani ambapo fedha zinazokusanywa ni kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa miundo mbinu na kuwezesha wakandarasi kulipwa kwa wakati.

**4) Mteja anapata Faida gani akiwekeza katika Hatifungani ya Miundombinu ya Samia?**
Kwa kuwekeza katika Hatifungani ya Miundombinu ya Samia, mwekezaji/mteja atapata:

- Usalama wa fedha katika kipindi chote cha uwekezaji
- Uhakika wa faida inayovutia katika kipindi kizima cha Hatifungani.
- Faida ya 12% kwa mwaka italipwa mara nne kwa mwaka na sio hadi muda wa hatifungani kuiva
- Mteja/mwekezaji hata katwa kodi kwenye faida anazopata.
- Fursa ya kuwekeza kwenye miradi ya kimkakati ya Serikali ambayo inaleta tija kwenye jamii.
- Ukihitaji fedha zako, kabla ya muda wa Hatifungani kuiva, unaweza kuuza hatifungani yako kupitia kwa Wakala wa Soko la Hisa (DSE) mwenye leseni ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA).
- Utaendelea kunufaika na kuponi uliyopata katika Hatifungani hadi muda utakapoamua kuziuza au muda wa kuiva kwake.

**5) Hatifungani ya Miundombinu ya Samia ni riba asilimia ngapi?**
Hatifungani ya Miundombinu ya Samia ina riba ya 12% kila mwaka. Inalipwa kila baada ya miezi 3 (robo mwaka)

CRDB BANK

# Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara (FAQs)

**6) Nani anaweza kuwekeza katika Hatifungani ya Miundombinu ya Samia?**

- Watu Binafsi (miaka 18 na Zaidi)
- Watoto (kupitia mzazi au mlezi)
- Vikundi,
- Mashirika/taasisi,
- Raia na wasio Raia wa Tanzania.
- Uwekezaji wa pamoja; mfano mke na mume

**7) Ni kiasi gani mwekezaji/mteja anahitaji kuwekeza katika Hatifungani ya Miundombinu ya Samia?**

Uwekezaji wa chini kabisa ni TZS 500,000 bila kikomo cha juu. Hata hivyo, mwekezaji anaweza kuendelea kuongeza uwekezaji wake katika Hatifungani ya Miundombinu ya Samia kupitia soko la upili, kwani dhamana hii imesajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE).

**8) Hatifungani ya Miundombinu ya Samia itaiva baada ya muda gani?**

Hatifungani ya Miundombinu ya Samia itaiva baada ya miaka 5

**9) Mwekezaji/Mteja atapokeaje kuponi na kiasi cha awali cha uwekezaji katika Hati Fungani ya Samia?**

Malipo yote yatafanywa moja kwa moja kwenye akaunti ya mwekezaji iliyojazwa katika fomu ya maombi ya Hatifungani ya Miundombinu ya Samia.

**10) Je, Mwekezaji/Mteja anaweza kujaza akaunti isiyo na jina lake kama akaunti ya kupokelea kuponi?**

Hapana, mwekezaji/mteja anapaswa kuweka akaunti yenye majina yake sahihi.

**11) Mteja anaweza kutumia Hatifungani yake kuomba mkopo?**

Ndio, mteja anaweza kutumia Hatifungani zake kuombea mkopo wenye thamani ya mpaka 80% ya Hatifungani zake na anaweza kutumia malipo yake ya kuponi kulipia mkopo wake

**12) Mwekezaji/Mteja anajiungaje na Hatifungani ya Miundombinu ya Samia?**

Ili kuwekeza katika Hatifungani ya Miundombinu ya Samia,

- Mwekezaji/Mteja Atajaza fomu ya maombi ya Hatifungani ya Miundombinu ya Samia inayotolewa na tawi la CRDB au wakala wa hisa. Taarifa muhimu zinazopaswa kutolewa kwenye fomu:
  - Taarifa za Mwekezaji na anuani halisi
  - Taarifa za akaunti ya benki itakayopokea Kuponi na kiasi cha awali.
  - Akaunti ya CDS (kama hauna akaunti ya CDS utafunguliwa)
- Mwekezaji atawasilisha nyaraka husika za utambulisho
- Kuweka kiasi cha uwekezaji cha TZS 500,000 au zaidi kwenye akaunti ya CRDB iliyotajwa kwenye fomu ya maombi

**13) Akaunti ya CDS ni nini?**

Akaunti ya CDS (Central Depository System) ni akaunti maalum inayotumika kuhifadhi na kusimamia hati za dhamana (kama hisa na Hatifungani) kwa njia ya kielektroniki. Akaunti

hii huanzishwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) na inaruhusu wawekezaji kununua, kuuza, na kuhamisha dhamana zao kwa urahisi zaidi na kwa usalama.

**14) Mwekezaji/Mteja anapataje akaunti ya CDS?**
Iwapo Mwekezaji/Mteja hana namba ya akaunti ya CDS, itafunguliwa kwa kutumia taarifa zilizojazwa na kwenye fomu yake ya maombi ya Hatifungani ya Miundombinu ya Samia.

**15) Je, Mwekezaji/Mteja anahitaji kuwa na akaunti ya benki na CRDB ili kuwekeza?**
Tunashauri mwekezaji/mteja kufungua akaunti na benki ya CRDB ambayo itarahisisha kupokea malipo ya kuponi.

**16) Je, Kiwango cha kuponi kinaweza kubadilika?**
Hapana, Kiwango cha kuponi (12% kwa mwaka) hakitobadilika katika kipindi chote cha uwekezaji.

**17) Mteja/Mwekezaji anawezaje kukokotoa Kuponi atakayolipwa?**
Kikokotoo kinapatikana kwenye tovuti ya **https://crdbbank-samiabond.mypage cloud.com/** Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya faida mabayo mteja tapata kwa kuwekeza viwango mbalimbali kwenye Hatifungani ya Miundombinu ya Samia.

## KIKOTOO CHA FAIDA

| | Riba ya Mwaka | | 12% | |
|---|---|---|---|---|
| | Kodi ya Zuio | | 0% | |
| Kiasi | Faida ya Jumla | | | |
| | Kila Robo Mwaka | Kila Nusu Mwaka | Kila Mwaka | Baada ya Ukomo (Miaka 5) |
| 5,000,000 | 150,000 | 300,000 | 600,000 | 3,000,000 |
| 10,000,000 | 300,000 | 600,000 | 1,200,000 | 6,000,000 |
| 20,000,000 | 600,000 | 1,200,000 | 2,400,000 | 12,000,000 |
| 50,000,000 | 1,500,000 | 3,000,000 | 6,000,000 | 30,000,000 |
| 100,000,000 | 3,000,000 | 6,000,000 | 12,000,000 | 60,000,000 |
| 500,000,000 | 15,000,000 | 30,000,000 | 60,000,000 | 300,000,000 |
| 1,000,000,000 | 30,000,000 | 60,000,000 | 120,000,000 | 600,000,000 |
| 5,000,000,000 | 150,000,000 | 300,000,000 | 600,000,000 | 3,000,000,000 |
| 10,000,000,000 | 300,000,000 | 600,000,000 | 1,200,000,000 | 6,000,000,000 |
| 100,000,000,000 | 3,000,000,000 | 6,000,000,000 | 12,000,000,000 | 60,000,000,000 |

**18) Je, Hatifungani ya Miundombinu ya Samia inapatikana kwa sarafu za kigeni?**
Hatifungani ya Miundombinu ya Samia inapatikana kwa shilingi ya kitanzania pekee. Iwapo mteja ana fedha za kigeni anashauriwa kuzibadilisha kwanza ili kupata shilingi za kitanzania kwa ajili ya kuwekeza kwenye Hatifungani ya Miundombinu ya Samia

# Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara (FAQs)

SAMIA INFRASTRUCTURE BOND

**19) Je, Mteja wa Hatifungani ya Miundombinu ya Samia anaweza kusitisha uwekezaji kabla ya tarehe ya kuiva?**
Hapana, uwekezaji ni kwa kipindi cha miaka 5. Hata hivyo, mwekezaji anaweza kuuza sehemu au kiasi chote cha uwekezaji wake katika Hatifungani ya Miundombinu ya Samia kupitia soko la upili, kwani dhamana hii imesajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE).

**20) Je, Mwekezaji/Mteja anaweza kuwa na Hatifungani ya Miundombinu ya Samia zaidi ya moja?**
Mteja atakuwa na hatifungani moja. Wakati wa mauzo ya awali, mteja ataweza kununua hatifungani ya Miundombinu ya Samia mara nyingi iwezekanavyo na itajumuishwa. Baada ya mauzo ya awali, mwekezaji anaweza kuongeza uwekezaji wake kwa kununua kupitia soko la upili, kwani dhamana hii imesajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE).

**21) Iwapo mmiliki wa Hatifungani ya Miundombinu ya Samia amefariki nini kitatokea?**
Umiliki wa Hatifungani ya Miundombinu ya Samia utahamishiwa kwa mrithi wa mali za marehemu aliyeidhinishwa kisheria.

**22) Je, Mwekezaji/Mteja atapata cheti cha umiliki wa Hatifungani?**
Ndio, Mteja/Mwekezaji atapata cheti cha umiliki Hatifungani.

**23) Raia wa kigeni anaweza kuwekeza kwenye Hatifungani ya Miundombinu ya Samia?**
Ndio, raia wa kigeni anaweza kuwekeza kwenye Hatifungani ya Miundombinu ya Samia

**24) Je, mteja anaweza kuchagua vipindi tofauti vya kupokelea kuponi zake?**
Hapana, utaratibu wa kupokea kuponi utakua ni kila baada ya miezi mitatu kama ilivyoidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA). Hata hivyo, mwekezaji anaweza kutumia bidhaa nyingine za kibenki zinazopatikana CRDB kutimiza matamanio yake ya upokeaji wa faida za uwekezaji wake.

**25) Je, mteja anawezaje kujiungana na Samia Bond?**
Mteja anaweza kujiunga na bondi kwa njia kuu mbili:
- Kupitia matawi ya CRDB
- Kwa kutumia huduma ya SimBanking

**26) Mwekezaji anaweza kuanza lini kuwekeza kwenye Hatifungani ya Miundombinu ya Samia?**
Ratiba ya uwekezaji kwenye Hatifungani ni kama ifuatavyo:

| TUKIO | TAREHE |
|---|---|
| Kufunguliwa kwa mauzo ya Hatifungani | 29 Novemba 2024 |
| Kufungwa kwa ofa | 17 Januari 2025 |
| Tarehe ya kusajiliwa kwenye Soko la Hisa | 10 Februari 2025 |
| Kuiva kwa Hatifungani | 10 Februari 2030 |

# Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara (FAQs)

**Kwa maelezo au maswali ya ziada tafadhali wasiliana na sisi kupitia;**
**Barua Pepe:** info@crdbbank.co.tz
**Namba ya simu:** +255(22)2197700 | +255(0)714197700 | +255(0)755197700 | 0800008000